# Curriculum design
# Kiswahili grade three

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Shambani** | Sauti mbili tofauti zinazotamkwa pamoja (*Vipindi 4*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbili zinazotamkwa pamoja ili kuimarisha matamshi bora<br>b) kutamka sauti lengwa ili kuimarisha matamshi bora<br>c) kusoma silabi za sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>d) kuandika silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha uandishi bora<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>f) kuandika maneno kutokana na silabi zilizofunzwa ili kuimarisha uandishi bora<br>g) kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kumsaidiwa mwanafunzi kutamka sauti husika ili kuimarisha matamshi na usomaji<br>h) kuchangamkia kutamka sauti lengwa ili kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi atambue sauti **bw**, **fy** na **kw** katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize silabi za sauti lengwa ikitamkwa na mwalimu kisha atamke pamoja na mwalimu na baadaye atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.Mifano ya silabi hizi ni: bwa, bwe; fya, fye; kwa, kwe, kwi n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza sauti lengwa ikitamkwa.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi k.v. silabi bwana, bweka, fyata, fyeka, kwao, kwea na kwekwe.<br>• Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni pamoja na maneno yanayojumuisha sauti hizo.<br>• Mwanafunzi asikilize imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika kupitia kwa mwalimu au vifaa vya teknolojia. | 1) Ni sauti zipi unazoweza kutamka?<br>2) Unajua kusoma sauti zipi mbili zinazotamkwa?<br>3) Unajua kuandika maneno gani yanayoundwa kutokana na sauti mbili zinazotamkwa pamoja? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati unaohusiana na shughuli za shambani ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma maneno na sentensi kuhusu shambani ili kuimarisha usomaji<br>c) kutunga sentensi akitumia msamiati wa shambani ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kuandika maneno na sentensi zinazojumuisha msamiati wa shambani katika kujenga uandishi bora<br>e) kuthamini matumizi ya msamiati wa shambani katika mawasiliano. | • Mwanafunzi asome msamiati wa shambani kama vile jembe, shoka, upanga, kifyekeo, plau, trekta, lima, fyeka, panda na kwekwe katika kadi na chati.<br>• Mwanafunzi ataje majina ya vifaa halisi, picha au michoro anavyoonyeshwa.<br>• Mwanafunzi atazame vifaa vya shambani hivyo kwenye tarakilishi au tabuleti vikifanya kazi.<br>• Mwanafunzi achore maumbo ya vifaa vinavyotumika shambani.<br>• Wanafunzi waambatanishe kadi za maneno na vifaa halisi wakiwa katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kushiriki katika nyimbo na mashairi kuhusu shambani.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya vifaa vinavyotumika shambani.<br>• Mwanafunzi atunge na kusoma sentensi akitumia msamiati wa shambani. | 1) Je, wajua vifaa vipi vinavyotumika shambani?<br>2) Ni kifaa kipi cha shamba unachoweza kuchora? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu shambani katika kujenga usikivu<br>b) kutaja majina ya vifa vinavyotumika shambani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kuelezea vifaa vinavyotumika shambani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza | • Mwanafunzi kusimulia kuhusu shambani.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu vifaa vinavyotumika shambani kama vile; jembe, shoka, upanga, kifyekeo, plau, trekta, lima, fyeka na panda akionyeshwa vifaa halisi, picha au michoro.<br>• Mwanafunzi aelezee umuhimu wa vifaa vinavyotumika shambani.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika nyimbo au mashairi kuhusu vifaa vinavyotumika shambani.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika kuigiza vitendo vinavyofanywa shambani. | 1) Je, ni vifaa vipi hutumika shambani?<br>2) Ni shughuli zipi zinazofanyika shambani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kuelezea shughuli zinazofanyika shambani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>e) kutambua matumizi ya vifaa vinavyotumika shambani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>f) kuthamini umuhimu wa vifaa vinavyotumika shambani. | • Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha jinsi vifaa mbalimbali vinavyotumika shambani<br>• Mwanafunzi anaweza kutumia tarakilishi kutambua vifaa mbalimbali kwa majina vilivyo. | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za vifaa vinavyotumika shambani ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>b) kusoma hadithi za picha zinazohusu shamba ili kujenga usomaji bora<br>c) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu vifaa vinavyotumika shambani ili kujenga usikivu<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu shambani ili kupata ujumbe<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi za vifaa vinavyotumika shambani ili kuendeleza stadi ya usomaji. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asome na wengine darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia k.m. tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wao baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kuhusu hadithi aliyosoma. | 1) Unaona nini katika picha?<br>2) Ni nini kitakachotendeka katika hadithi?<br>3) Ni vifaa vipi vimetajwa katika hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka mwingine.<br>• Mwanafunzi aelezee yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, ni kisa gani unachoweza kuandika juu ya shamba? |
| | Sarufi: Nafsi ya tatu wakati ujao-umoja na wingi<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno na viambishi vinavyotumika kuonyesha nafsi ya tatu na wakati ujao katika umoja na wingi ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutumia nafsi ya tatu wakati ujao hali ya umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma vifungu vilivyo na nafsi ya tatu, wakati ujao kwa umoja na wingi ili kujenga usomaji<br>d) kuandika vifungu vilivyo na nafsi ya tatu, wakati ujao kwa umoja na wingi ili kujenga uandishi bora | • Mwanafunzi atumie nafsi ya tatu wakati ujao hali ya umoja na wingi katika mazungumzo.<br>• Mwanafunzi atumie nafsi ya tatu wakati ujao hali ya umoja na wingi katika sentensi.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia nafsi ya tatu wakati ujao hali ya umoja na wingi.<br>• Wanafunzi wanaweza kupewa sentensi zinazojumuisha nafsi na nyakati mbalimbali wazitambue katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi katika tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura na kutia kapuni.<br>• Mwanafunzi aigize vitendo vya kuashiria nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu huku akitunga sentensi.<br>• Mwanafunzi aweza kupata ufafanuzi wa nafsi kwa kutumia vibonzo katika tarakilishi. | 1) Je, unatumia neno gani kuonyeshea mwenzako akiwa mbali?<br>2) Ikiwa nanuia kusafiri kesho, nitasemaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kufurahia kutumia nafsi ya tatu wakati ujao hali ya umoja na wingi katika mawasiliano. | | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – Wanatumia lugha faafu darasani. Vilevile wanashirikiana katika kazi ya vikundi.
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.
ubunifu: mwanafunzi napoandika au kusimulia kisa
kufikiria kwa kina na kutatua changamoto – mwanafunzi anapojibu maswali ambayo majibu yake hayapatikani moja kwa moja kutoka kwenye kisa
hamu ya ujifuzaji – mwanafunzi atapata hamu ya kutaka kujua matumizi ya vifaa vya shambani.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>elimu ya maendeleo endelevu: athari za majanga – kujua athari za vifaa vya shambani<br>uraia : kuthamini kilimo katika kukuza uchumi wa nchi. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji wa kutunza vifaa vya shambani<br>kutunza vifaa vya shambani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kushiriki katika ukulima nyumbani. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kushiriki katika vikundi vya ushirika shuleni vinavyohusu ukulima<br>kushuriki katika kilimo shuleni. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa shambani katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia nafsi ya tatu wakati ujao katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa kwa ufasaha<br>• anasimulia shughuli zinazofanyika shambani kwa ubunifu | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo<br>• anasimulia shughuli zinazofanyika shambani | Mwanafunzi,<br>• anatamka baadhi ya sauti ipasavyo<br>• anasimulia baadhi ya shughuli za shambani | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutamka sauti alizofunzwa<br>• ana changamoto katika kusimulia shughuli za shambani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anasoma hadithi kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anaandika kisa kifupi kwa hati nadhifu na ubunifu<br>• anatunga sentensi sahihi akizingatia nafsi ya tatu wakati ujao katika umoja na wingi kila wakati. | • anasoma hadithi kwa ufasaha.<br>• anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anaandika kisa kifupi kwa hati bora<br>• anatunga sentensi sahihi akizingatia nafsi ya tatu wakati ujao katika umoja na wingi. | • anasoma hadithi kwa ufasaha<br>• ana chamgamoto kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anajaribu kuandika kisa kwa hati inayosomeka<br>• ana changamoto kutunga sentensi sahihi akizingatia nafsi ya tatu wakati ujao katika umoja na wingi. | • ana changamoto katika kusoma hadithi<br>• ana chamgamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kuandika kisa<br>• ana changamoto kutunga sentensi sahihi akizingatia nafsi ya tatu wakati ujao katika umoja na wingi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Uzalendo** | Sauti mbili tofauti zinazotamkwa pamoja (*Vipindi 5*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbili zinazotamkwa pamoja ili kuimarisha matamshi bora<br>b) kutamka sauti lengwa ili kuimarisha matamshi bora<br>c) kusoma silabi za sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>d) kuandika silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha uandishi bora<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>f) kuandika maneno kutokana na silabi zilizofunzwa ili kuimarisha uandishi | • Mwanafunzi atambue sauti **mw**, **nd** na **pw** katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akizitamka silabi zinazotokana na sauti lengwa kisha atamke pamoja na mwalimu na baadaye atamke akiwa pekee, wawili na darasa zima k.m mwa, mwe, mwi na mwo.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia kama vile papaya, tarakilishi, projekta na kipaza sauti kumsaidia kuimarisha matamshi yake.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno kwa mfano k. m mwana, mwananchi, ndoo, ndizi, uzalendo, pwani, pweza na pweke. | 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma silabi zipi katika maneno?<br>3) Ni herufi na maneno yapi yanayoundwa kutokana na sauti mbili zinazotamkwa pamoja? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | bora<br>g) kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kumsaidia mwanafunzi kutamka sauti husika ili kuimarisha matamshi na usomaji<br>h) kuchangamkia kutamka sauti lengwa ili kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kugawa yaliyo marefu zaidi katika sehemu ndogo ndogo.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa darasani au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa.<br>• Mwanafunzi aandike maneno yanayojumuisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asikilize imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. | |
| | Msamiati.<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati ambao unahusiana na uzalendo ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma msamiati unaohusiana na uzalendo ili kujenga usomaji<br>c) kueleza maana ya msamiati wa uzalendo ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kutumia msamiati wa uzalendo katika sentensi sahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>e) kuandika maneno yanayohusiana na uzalendo ili kuimarisha uandishi bora<br>f) kuthamini uzalendo ili kuwa mzalendo kwa nchi yake. | • Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na uzalendo kama vile; umoja, amani, upendo, bendera, taifa, nchi, raia, gwaride, rangi za bendera kwa kutumia kadi za maneno.<br>• Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati wa uzalendo.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu maana za maneno yanayohusiana na uzalendo<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa uzalendo.<br>• Wanafunzi watazame video kuhusu vitendo vya kizalendo k.m. mashujaa wa nchi.<br>• Mwanafunzi atazame michoro na picha inayolenga maana za maneno kuhusu uzalendo.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa uzalendo wakiwa kwenye vikundi. | 1) Je, uzalendo ni nini?<br>2) Unajua maneno yapi yanayohusiana na uzalendo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayoonyesha uzalendo ili kuyatumia katika mawasiliano<br>b) kusimulia visa vinavyojumuisha mambo yanayoweza kuimarisha uzalendo ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>c) kusikiliza masimulizi kuhusu uzalendo ili kuimarisha usikivu<br>d) kuthamini umuhimu wa uzalendo katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi aeleze baadhi ya mambo yanayoweza kuimarisha uzalendo katika nchi yake kwa kutumia mgeni mwalikwa.<br>• Mwanafunzi asimulie visa vinavyojumuisha mambo yanayoweza kuimarisha uzalendo kama vile amani, umoja, upendo na bendera ya Kenya.<br>• Mwanafunzi asikilize kwa makini hadithi anazosimuliwa.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha vitendo vya kizalendo.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu uzalendo katika makundi.<br>• Wanafunzi waimbe wimbo wa taifa na kujadili maana ya baadhi ya maneno ya kizalendo katika wimbo huo.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi kuhusu baadhi ya mambo yanayohusu uzalendo.<br>• Mwanafunzi ataje baadhi ya sifa za mzalendo kama vile kupenda nchi yake, amani na umoja. | 1) Je, ni nini maana ya uzalendo?<br>2) Uzalendo una umuhimu gani?<br>3) Je, ni kwa njia zipi unaweza kuonyesha uzalendo?<br>4) Bendera ina umuhimu gani? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua rangi za bendera ili kuimarisha uzalendo<br>b) kutambua maneno yanayohusiana na uzalendo ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma hadithi za kizalendo ili kujenga usomaji<br>d) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu uzalendo ili kuimarisha usikivu | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi kama vile amani, umoja, upendo, nchi, taifa, raia, bendera na wimbo wa taifa.<br>• Wanafunzi washiriki kusoma katika darasa, wakiwa wawili, kwenye vikundi au asome peke yake. | 1) Je, unajua nini kuhusu uzalendo?<br>2) Ni vipi unavyoweza kuonyesha upendo kwa nchi yako?<br>3) Sifa za mzalendo ni zipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu uzalendo ili kupata ujumbe<br>f) kuthamini umuhimu wa uzalendo katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa kupitia kinasasauti.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi ule.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuulizwa maswali kutokana na hadithi aliyosoma au kusomewa. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aelezee yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, ni tukio gani unaloweza kukumbuka na kuandikia kisa? |
| | Sarufi<br>(Matumizi ya: **-ake** na **-ao**)<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya; **-ake** na **–ao** ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma vifungu vya maneno vinavyojumuisha **-ake** na **-ao** ili kujenga usomaji<br>c) kutunga sentensi akitumia **-ake** na **-ao** ili kuimarisha ubunifu | • Mwanafunzi aonyeshe vitu vyake na vya wengine darasani na kuvirejelea akitumia **-ake** na **–ao.**<br>• Mwanafunzi asome vifungu vyenye matumizi **-ake** na **–ao.**<br>• Mwananafunzi akamilishe vifungu kwa kutumia **-ake** na **–ao** km Kalamu _______ (kalamu yake)- Kalamu ______ (Kalamu zao); kitabu ______ (Kitabu chako) – Kitabu ______(Vitabu vyao).<br>• Mwanafunzi atunge sentensi kwa kutumia **–ake** na **–ao**. | 1) Je, utatumia neno gani kuonyesha kwamba unachozungumzia ni chako?<br>2) Je, ni nini wingi wa **–ake**? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>d) kuandika sentensi akitumia akitumia<br>**-ake** na **-ao** ili kujenga uandishi bora<br>e) kuchangamkia kurejelea vitu vyake na vya wenzake akitumia **-ake** na **-ao** katika mawasiliano ya kila siku.</td><td>• Mwanafunzi aweza kutumia tarakilishi kufanya zoezi.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>uraia: uzalendo – kushiriki katika kuimba wimbo wa taifa<br>mawasiliano na ushirikiano – kushirikiana pamoja darasani<br>kifikiri kwa kina na kutatua changamoto – Katika kujibu maswali ya ufahamu yasiyo na majibu ya moja kwa moja<br>ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.</td></tr>
<tr><td colspan="3">**Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>uraia: uzalendo – kushiriki katika kuimba wimbo wa taifa.</td><td colspan="2">**Uhusiano na Maadili:** umoja, uzalendo, haki za kijamii, uwajibikaji, mapenzi kwa nchi, heshima na amani.</td></tr>
<tr><td colspan="3">**Uhusiano na masomo mengine:** Environmental Activities, Movement and Creative Activities.</td><td colspan="2">**Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kushiriki katika kuimba nyimbo zinazokuza uzalendo katika sherehe mbalimbali.</td></tr>
<tr><td colspan="3">**Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kushiriki katika uskauti shuleni<br>kupandisha bendera shuleni<br>kushuriki katika kuimba wimbo wa taifa.</td><td colspan="2">**Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa shambani katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia –ake na -ao katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kufuatilia mwandiko wake<br>• kuchunguza anavyotumia lugha katika masimulizi.</td></tr>
</table>

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo na kwa ufasaha<br>• anasimulia visa vinavyohusiana na uzalendo kwa ubunifu<br>• anasoma hadithi kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatunga sentensi sahihi akitumia **–ake** na **-ao** kila wakati<br>• anaandika kisa kifupi kwa hati nadhifu, ubunifu, mtiririko mwafaka na kwa haraka. | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo<br>• anasimulia visa vinavyohusiana na uzalendo<br>• anasoma hadithi kwa ufasaha<br>• anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatunga sentensi sahihi akitumia –**ake** na **-ao**<br>• anaandika kisa kifupi kwa hati bora na kwa mtiririko ufaao. | Mwanafunzi,<br>• anatamka baadhi ya sauti ipasavyo<br>• anasimulia visa vinavyohusiana na uzalendo.<br>• anasoma hadithi<br>• anafahamu baadhi ya hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto kutunga sentensi sahihi akitumia **–ake** na **-ao**<br>• anajaribu kuandika kisa kifupi kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto kutamka sauti ipasavyo<br>• ana changamoto kusimulia visa vinavyohusiana na uzalendo<br>• ana changamoto kusoma hadithi<br>• ana changamoto kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto kutunga sentensi sahihi akitumia **–ake** na **-ao**<br>• ana changamoto katika kuandika kisa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MADA NDOGO |
|---|---|---|---|---|
| **Miezi ya Mwaka** | Sauti mbili tofauti zinazotamkwa pamoja (*Vipindi 4*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbili zinazotamkwa pamoja ili kuimarisha matamshi bora<br>b) kutamka sauti lengwa ili kuimarisha matamshi bora<br>c) kusoma silabi za sauti lengwa ili kuimarisha usomaji | • Mwanafunzi atambue sauti **mb**, **nj** na **ng** katika maneno.<br>• Mwanafunzi amsikilize mwalimu akitamka silabi zinazotokana na sauti lengwa kisha atamke. pamoja na mwalimu na baadaye atamke akiwa pekee, wawili na darasa zima. Mifano ya silabi hizi ni: mba, mbe, mbi,nja, nje, nji, nga, nge na ngi.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya ki teknolojia kama vile papaya, tarakilishi, projekta na kipazasauti | 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma herufi zipi?<br>3) Unajua kuandika herufi na maneno kutokana na sauti mbili |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>e) kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kumsaidia mwanafunzi kutamka sauti husika katika kuimarisha matamshi na usomaji<br>f) kuandika silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha uandishi bora<br>g) kuandika maneno kutokana na silabi zilizofunzwa ili kuimarisha uandishi bora<br>h) kuchangamkia kutamka sauti lengwa ili kuimarisha mawasiliano. | katika kuimarisha matamshi yake.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosikia katika maneno kwa mfano k. m mbuzi, mbuni, Septemba, Disemba, njugu, ngazi na funga<br>• Mwanafunzi aandike maneno yanayojumuisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kuunganisha silabi na kugawa maneno yaliyo marefu zaidi katika sehemu ndogo ndogo.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa darasani au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi asikilize imla ya maneno yenye silabi za sauti lengwa na kuyaandika. | zinazotamkwa pamoja? |
| | Msamiati: Majina ya miezi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miezi ya mwaka ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kusoma majina ya miezi ya mwaka ili kuimarisha usomaji bora<br>c) kuandika majina ya miezi ya mwaka kwa mfuatano ili kujenga uandishi bora<br>d) kutumia majina ya miezi katika sentensi ili kujenga ubunifu<br>e) kuchangamkia majina ya miezi katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi asome majina ya miezi ya mwaka ipasavyo kwa kutumia kadi za maneno.<br>• Wanafunzi waweza kukariri mashairi yanayohusu miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo zinazohusu miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya miezi ya mwaka.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa katika kupanga upya majina miezi ya mwaka yaliyoparaganywa.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia majina ya miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa vibonzo vikitaja miezi ya mwaka na kuelezea matukio tofauti ya mwaka. | 1) Je, unajua majina yapi ya miezi?<br>2) Je, ulizaliwa mwezi gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua majina ya miezi ya mwaka kwa Kiswahili ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutaja miezi ya mwaka kwa Kiswahili ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kusikiliza masimulizi kuhusu miezi ya mwaka ili kujenga usikivu<br>d) kuthamini umuhimu miezi ya mwaka maishani. | • Mwanafunzi ataje miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi aweza kuelezea mambo yanayofanyika miezi fulani kv kufungua shule mwezi wa Januari, kufunga shule mwezi wa Aprili.<br>• Mwanafunzi asimulie kuhusu matukio katika miezi mbalimbali k.v. kuzaliwa, shehere za kidini na kitaifa.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi asome majina ya miezi ya mwaka kupitia kwa vifaa kama kadi za majina.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu shughuli zinazofanyika katika miezi tofauti tofauti.<br>• Mwanafunzi amsomee mwenzake au asomee kikundi, majina ya miezi ya mwaka.<br>• Wanafunzi waweza kupewa kadi zilizo na matukio mbalimbali ya mwaka waambatanishe na miezi yenyewe katika makundi.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya miezi ya mwaka.<br>• Mwanafunzi aweza kufuatanisha majina ya miezi ya mwaka. | 1) Unajua miezi gani ya mwaka?<br>2) Je, ulizaliwa mwezi gani?<br>3) Mwaka una miezi mingapi?<br>4) Ni mwezi upi wa mwaka huwa na sherehe nyingi? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu inayojumuisha miezi ili kuimarisha stadi za kusikiliza na kusoma<br>b) kusoma hadithi zinazojumuisha miezi na nambari ili kuimarisha usomaji | • Mwanafunzi asikilize mwalimu akisoma hadithi.<br>• Mwanafunzi asome hadithi peke yake.<br>• Wanafunzi wasomeane hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ambapo hadithi inasomwa.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu lililowekwa mbele ya darasa. | 1) Je, ni hadithi gani uliyofurahia ukisomewa?<br>2) Je, waweza kukumbuka nini ulichosoma au kusomewa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu miezi ya mwaka ili kupata ujumbe<br>d) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kuhusu hadithi aliyosoma.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka<br>• Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa kipi kuhusu jambo ulilofanya katika mwezi fulani wa mwaka? |
| | Msamiati: Tarakimu 51-100<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua nambari 51-100 kwa maneno ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kusoma nambari 51-100 kwa maneno ili kuimarisha usomaji bora<br>c) kuandika nambari 51- 100 kwa maneno ili kuimarisha uandishi bora<br>d) kuchangamkia kutumia nambari 51 – 100 kwa maneno katika mazungumzo yake. | • Mwanafunzi asome majina ya nambari 51-100<br>• Wanafunzi waweza kupatiwa kadi za nambari 51-100 na majina yake ili kuziambatanisha katika makundi.<br>• Mwanafunzi aandike nambari 51-100.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kupanga upya majina yaliparaganywa ya nambari 51-100.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia nambari 51-100.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa vibonzo vikihesabu hadi 100 kwenye tarakilishi. | 1) Unaweza kuandika nambari zipi?<br>2) Unaweza kutumia nambari gani kati ya 51-100 katika sentensi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Sarufi:<br>Matumizi ya Kikomo<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua matumizi ya kikomo (.) katika kuimarisha mawasiliano<br>b) kuakifisha sentensi kwa kutumia kikomo(.) katika kuimarisha uandishi bora<br>c) kuzingatia kikomo (.) anaposoma kifungu na sentensi ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kuthamini matumizi ya kikomo (.) katika mawasiliano. | • Mwanafunzi asome sentensi zenye kikomo (.) katika vikundi<br>• Mwanafunzi aakifishe sentensi fupi kwa kutumia kikomo (.).<br>• Mwanafunzi aandike sentensi ukitumia kikomo (.). | 1) Unajua alama zipi za kuakifisha?<br>2) Je, kikomo (.) huwekwa wapi katika sentensi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – kushirikiana pamoja darasani
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>elimu ya kudumisha maendeleo: elimu ya maswala ya fedha: kujua kuratibu shughuli za kila siku. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji<br>uzalendo (katika kukumbuka miezi na siku za sherehe za kitaifa). |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mathematics Activities, Environmental Activities na English Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kushiriki katika kuratibu shughuli zinazoendeshwa katika jamii. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kuzingatia ratiba ya shule inayoonyesha shughuli za miezi mbalimbali. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa miezi ya mwaka na tarakimu katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia alama ya kikomo katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kufuatilia mwandiko wake<br>• kuchunguza anavyotumia lugha katika masimulizi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi;<br>• anatamka sauti kwa haraka na ipasavyo<br>• anasimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka kwa ubunifu<br>• anasoma hadithi kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anaandika sentensi akitumia kikomo kila siku<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko na hati nadhifu na kwa haraka. | Mwanafunzi;<br>• anatamka sauti ipasavyo<br>• anasimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka kwa ubunifu<br>• anasoma hadithi kwa ufasaha<br>• anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anaandika sentensi akitumia kikomo<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. | Mwanafunzi;<br>• anatamka baadhi ya sauti ipasavyo<br>• anasimulia baadhi ya hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka<br>• anasoma hadithi<br>• anafahamu baadhi ya hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anaandika baadhi ya sentensi akitumia kikomo<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi;<br>• anatamka baadhi ya sauti<br>• ana changamoto katika kusimulia hadithi zinazojumuisha miezi ya mwaka<br>• anasoma baadhi ya hadithi japo bila ufasaha ufaao<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kuandika sentensi akitumia kikomo<br>• ana changamoto katika kuandika kisa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Kazi mbalimbali** | Sauti mbili tofauti zinazotamkwa pamoja (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbili zinazotamkwa pamoja ili kuimarisha matamshi bora<br>b) kutamka sauti lengwa ili kuimarisha matamshi bora<br>c) kusoma silabi za sauti lengwa ili | • Mwanafunzi atambue sauti **py** na **vy** katika maneno<br>• Mwanafunzi amsikilize mwalimu akitamka silabi zinazotokana na sauti lengwa kisha atamke pamoja na mwalimu na baadaye atamke akiwa pekee, wawili na darasa zima k.m pya, pye, vya na vye.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia kama vile papaya, tarakilishi, projekta na kipazasauti ili kuimarisha | 1) Je, ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Je, ni sauti zipi zinazokutatiza kutamka?<br>3) Je, ni sauti zipi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha usomaji<br>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji<br>e) kusoma kwa sauti hadithi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha matamshi na usomaji<br>f) kuandika silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha uandishi bora<br>g) kuandika maneno kutokana na silabi zilizofunzwa ili kuimarisha uandishi bora<br>h) kuchangamkia kutamka sauti lengwa ili kuimarisha mawasiliano. | matamshi yake.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno kwa mfano k. m mpya, kipya, kompyuta, vyema, vyoo na vyote.<br>• Mwanafunzi aandike maneno yanayojumuisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuyagawa yaliyo marefu zaidi katika sehemu ndogo ndogo.<br>• Wanafunzi waweza kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa darasani au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi asikilize imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. | unazotamka bila shida? |
| | Msamiati<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa kazi mbalimbali ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutunga sentensi akitumia msamiati wa kazi mbalimbali ili kujenga ubunifu<br>c) kusoma maneno na sentensi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usomaji<br>d) kuandika maneno na sentensi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha uandishi | • Mwanafunzi atazame picha, michoro au DVD inayoonyesha watu na kazi mbalimbali k.v ualimu, ukulima, udaktari, uyaya, unesi na ubawabu ili azitambue peke yake au katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kuambatanisha kadi za maneno na kazi mbalimbali wakiwa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aeleze kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi asome msamiati wa kazi mbalimbali katika kadi, chati nk.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi kuhusu kazi mbalimbali<br>• Mwanafunzi atunge na kusoma sentensi akitumia msamiati wa kazi mbalimbali. | 1) Ni neno gani unaloweza kusoma kwenye kadi?<br>2) Ni kazi ipi unayoipenda?<br>3) Kwa nini watu hufanya kazi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuthamini kazi mbalimbali ili kutambua huduma zinazotolea na watu wanaofanya kazi mbalimbali. | | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usikivu<br>b) kuelezea kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kutaja majina ya kazi mbalimbali na watu wanaozifanya ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d) kuthamini kazi mbalimbali. | • Mwanafunzi asimulie kuhusu kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi eleze umuhimu wa kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi aweza kushiriki katika nyimbo au mashairi kuhusu kazi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kuigiza kazi inayofanywa na watu mbalimbali.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa anapozungumzia kuhusu kazi mbalimbali.<br>• Wanafunzi waweza kutazama picha au michoro inayoonyesha watu na kazi mbalimbali wajadiliane katika vikundi. | 1) Ni kazi zipi unazozijua?<br>2) kazi unazozijua zina umuhimu gani? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za watu na kazi mbalimbali ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>b) kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usomaji na usikivu<br>c) kusoma hadithi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Wanafunzi waweza kusoma katika darasa, wakiwa wawili na baadaye mwanafunzi asome peke yake.<br>• Mwanafunzi anaweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. | 1) Unaona nini kwenye picha?<br>2) Ni aina gani ya kazi ambayo imewasilishwa kwenye picha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu kazi mbalimbali ili kupata ujumbe<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi. | • Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza kuhusu hadithi aliyosoma. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa.<br>• Wanafunzi waweza wakaandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa gani kifupi kinachohusiana na kazi yoyote? |
| | Sarufi:<br>Ukanusho wa nyakati<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua ukanusho wa **-li-**; **-na-**; **-ta-** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kuimarisha usomaji<br>c) kuandika ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kujenga ubunifu<br>d) kuchangamkia matumizi ya nyakati katika mawasiliano. | • Wanafunzi watumie **-li-**; **-na-**; **-ta-** kuelezea vitendo walivyofanya katika wakati uliopita (LI), ulipo (NA) na ujao (TA) wakiwa katika vikundi au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi akamilishe vifungu kwa kutumia **-li-**; **-na-**; **-ta-** na ukanusho wake.<br>• Mwanafunzi asome vifungu vyenye matumizi **-li-**; **-na-**; **-ta-** na ukanusho wake.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la ukanusho wa nyakati akiwa peke yake, wawili wawili au katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama jinsi nyakati zinavyokanushwa katika vifaa vya kiteknolojia na kufanyia zoezi kwenye mtandao. | 1) Unafanya nini sasa?<br>2) Ulifanya nini jana?<br>3) Utafanya nini kesho?<br>4) Je, ni nyakati zipi ambazo unajua kukanusha? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>mawasiliano na ushirikiano – kushirikiana kufanya kazi katika vikundi<br>kujiamini/kujithamini – kuthamini na kutambua kazi mbalimbali; Kujibu maswali ya kisarufi vilivyo<br>ubunifu – Katika utunzi wa sentensi na kujibu maswali ya ufahamu ambayo majibu yake si ya moja kwa moja<br>ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>shughuli zinazomsaidia mwanafunzi: mwongozo wa ajira – kuthamini kazi mbalimbali<br>stadi za Maisha – ujuzi wa kazi mbalimbali na umuhimu wake.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>uwajibikaji; uzalendo; umoja na heshima</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine: Engilish Activities, Environmental Activities</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji: kusaidia wazazi katika kazi za nyumbani na katika jamii<br>kuthamini kazi zinazofanywa na wazazi, ndugu na watu wengine katika jamii.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:<br>kushiriki katika kuigiza, kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali.</td><td colspan="2">Mapendekezo ya Tathmini:<br>• kuhakiki matamshi ya sauti mbili zinazotamkwa pamoja<br>• kuchunguza anavyotambua kazi mbalimbali<br>• kuchunguza anavyotumia ukanusho wa nyakati katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kufuatilia mwandiko wake.</td></tr>
</table>

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo na kwa ufasaha<br>• anaelezea kuhusu kazi mbalimbali kwa ufasaha.<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo.<br>• anaelezea kuhusu kazi mbalimbali<br>• anasoma maneno, sentensi na | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti ipasavyo<br>• anataja kazi mbalimbali<br>• anasoma baadhi ya maneno, sentensi na | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto kutamka sauti<br>• ana changamoto kuelezea kuhusu kazi mbalimbali<br>• ana changamoto katika kusoma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia kikomo ipasavyo<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. | hadithi kwa ufasaha<br>• anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia kikomo ipasavyo<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. | hadithi vilivyo<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosoma au kusomewa.<br>• anatumia kikomo<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | maneno, sentensi na hadithi<br>• anachangamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia kikomo<br>• ana changamoto katika kuandika kisa kuhusu mada aliyopewa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Usalama** | Msamiati.<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika usalama ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma msamiati unaohusiana na usalama ili kujenga usomaji bora<br>c) kueleza maana ya msamiati wa usalama ili kuimarisha ufahamu<br>d) kutumia msamiati wa usalama katika sentensi ili kuimarisha ufahamu<br>e) kuandika maneno yanayohusiana na usalama ili kujenga uandishi bora<br>f) kuthamini usalama katika mazingira yake. | • Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno.<br>• Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati wa usalama akiwa peke yake au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa usalama.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usalama k.m. utekaji nyara na moto na kisha kujadili jinsi ya kujilinda kutokana na hatari.<br>• Mwanafunzi atazame michoro na picha inayolenga maana ya maneno kuhusu usalama.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa usalama. | 1) Je, ni nini maana usalama?<br>2) Usalama huhusisha mambo yapi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Maagano (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweza:<br>a) kutambua maneno yanayotumiwa katika maagano ili kuwezesha mazungumzo<br>b) kutumia maneno yanayotumiwa katika maagano kwenye mawasiliano<br>c) kujibu maagano kwa njia ifaayo ili kudhihirisha ufahamu<br>d) kuthamini matumizi ya maagano katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi anaweza kueleza matumizi ya maagano kama vile: kwaheri; siku njema, mchana mwema, safiri salama na usiku mwema.<br>• Mwanafunzi atazame michoro inayoashiria vitendo vya kuagana.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika maigizo ya kuagana.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama vibonzo katika tarakilishi vikiigiza vitendo na maneno mbalimbali ya kuagana.<br>• Mwanafunzi aweza kutaja neno la kuagana linalofaa kutokana na maelezo mbalimbali akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. | 1) Je, ulipoagana na mzazi asubuhi alikwambiaje?<br>2) Je, mzazi hukwambiaje unapoenda kulala?<br>3) Mtu anaposafiri anaambiwaje? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo yanayoathiri usalama ili kujihakikishia usalama<br>b) kutambua njia za kudumisha usalama katika mazingira yake ili kujihakikishia usalama<br>c) kusimulia kuhusu mambo yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d) kusikiliza masimulizi kuhusu usalama ili kujenga stadi ya kusikiliza<br>e) kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi asimulie baadhi ya mambo. yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake kupitia k.m. mgeni mwalikwa.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake.<br>• Wanafunzi wajadiliane namna ya kuepuka dhuluma k.m. kutozungumza na watu wasiowajua, kupiga ukelele anapokumbwa na hatari.<br>• Mwanafunzi aandike baadhi ya mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake.<br>• Mwanafunzi asimulie kisa alichokishuhudia kuhusu usalama. | 1) Usalama ni nini?<br>2) Usalama unatusaidia na nini?<br>3) Unaweza ukafanya nini unapovamiwa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha zinazoonyesha usalama katika mazingira mbalimbali ili kurahisisha ufahamu<br>b) kutambua maneno yanayohusiana na usalama ili kuyatumia katika mawasiliano<br>c) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu usalama ili kuimarisha ufahamu<br>d) kusoma hadithi kuhusu usalama ili kujenga usikivu<br>e) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu usalama ili kupata ujumbe<br>f) kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asome darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Wanafunzi wasomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa kupitia kinasa sauti.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu mzima au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi huo.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu usalama.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. | 1) Je, usalama unahusu nini?<br>2) Ukosefu wa salama husababishwa na nini?<br>3) Unapojipata kwenye hatari unafaa kufanya nini? |
| | Kuandika ( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kisa chenye mtiririko<br>b) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada<br>c) kufurahia uandishi wa visa tofauti | • Mwanafunzi aweza kupewa hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aongozwe kujadili yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma kielelezo cha kisa | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa gani |



**Compiled and Distributed by Schools Net Kenya | P.O.BOX 85726 – 00200, NAIROBI |**
**Mob: 0725788400 | Email:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | maishani. | kilichoandikwa.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi apewe fursa ya kuandika kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | kifupi kinachohusiana na usalama? |
| | Sarufi: Vinyume vya vitendo (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutaja vinyume vya vitendo<br>b) kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo<br>c) kuandika vinyume vya vitendo<br>d) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aweza kufafanuliwa juu ya vinyume vya vitendo kama vile lala-amka; keti- simama; cheka-lia; tabasamu – nuna; enda-rudi; panda – shuka nk.<br>• Wanafunzi waweza kuigiza vinyume vya vitendo wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa kutunga na kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo.<br>• Mwanafunzi aweza kuelekezwa kuandika vinyume vya vitendo. | 1) Je, unajua vinyume vya vitendo unavyofanya kila siku? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawisiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza
ubunifu – unadhihirishwa na usimulizi na utungaji wa sentensi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya usalama – kupitia kwa kutambua umuhimu na mbinu za kujilinda na hali zinazohatarisha usalama<br>Stadi za maisha – mbinu za kujilinda dhidi ya tisho kwa usalama wake. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji -kuwa na msimamo thabiti katika uamuzi wake<br>haki za kijamii- kufuata haki zake anapodhulumiwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental Activities; Hygiene and Nutrition; English Activities. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kusaidia kuhamasisha jamii kuhusu usalama<br>kushiriki katika kutetea haki za kijamii. |

| | |
|---|---|
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>Kushiriki katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali kuhusu usalama. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa usalama katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia vinyume vya vitendo katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatambua na kutumia mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake<br>• anatumia maneno ya maagano ifaavyo kila wakati<br>• anasimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama kwa ubunifu na ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anaandika vinyume vya vitendo kwa usahihi<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. | Mwanafunzi,<br>• anatambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake<br>• anatumia maneno ya maagano ifaavyo<br>• anasimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama kwa ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha<br>• anaandika vinyume vya vitendo kwa usahihi<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. | Mwanafunzi,<br>• anatambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake<br>• anatumia maneno ya maagano ifaavyo<br>• anaelezea kuhusu kisa alichoshuhudia bila mtiriko wenye mantiki<br>• anasoma maneno, sentensi na baadhi ya hadithi kwa ufasaha<br>• ana changamoto kuandika vinyume vya baadhi ya vitendo kwa usahihi<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto kutambua mbinu mbalimbali za kujiepusha na hali zinazoweza kuhatarisha usalama wake<br>• ana changamoto katika kutumia baadhi ya maneno ya maagano katika mawasiliano<br>• ana changamoto kusimulia kisa alichokishuhudia kuhusu usalama<br>• ana changamoto kusoma maneno, sentensi na hadithi kwa ufasaha<br>• ana changamoto kuandika vinyume vya vitendo kwa usahihi<br>• ana changamoto kuandika kisa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Usafi wa Mazingira** | Msamiati ( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa usafi wa mazingira<br>b) kutumia msamiati wa usafi wa mazingira katika sentensi<br>c) kubainisha mazingira safi na yale machafu<br>d) kuthamini mazingira safi. | • Mwanafunzi aweza kuelekezwa kusoma maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kuelekezwa kutoa maana ya msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu maana za maneno yanayohusiana na usafi wa mazingira.<br>• Mwanafunzi aweza kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usafi wa mazingira k.m. kuokota na kuchoma taka, kufyeka nyasi n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha zinazolenga maana ya maneno kuhusu usafi wa mazingira.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira wakiwa kwenye vikundi. | 1) Je, unajua msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira?<br>2) Unaweza kutumia msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira sentensi?<br>3) Mazingira safi ni yapi? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutofautisha mazingira safi na yasiyo safi<br>b) kutambua umuhimu wa mazingira safi<br>c) kusikiliza masimulizi kuhusu usafi wa mazingira<br>d) kuelezea kuhusu usafi wa mazingira | • Mwanafunzi aweza kufahamu maana ya usafi wa mazingira.<br>• Wanafunzi waongozwe katika vikundi kusimulia visa vinavyohusiana na usafi wa mazingira k.v. umuhimu na jinsi ya kutunza mazingira<br>• Mwanafunzi aweza kuigiza jinsi ya kudumisha usafi katika mazingira yake<br>• Wanafunzi waweza kutazama video inayohusu mazingira safi na chafu kisha wabainishe mazingira | 1) Ni nini maana ya mazingira?<br>2) Mazingira safi ni yapi?<br>3) Je, tunawezaje kuborasha mazingira? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuelezea jinsi ya kutunza mazingira yake<br>f) kufurahia mazingira safi maishani mwake. | wanayofurahia.<br>• Mwanafunzi anaweza kuchora vifaa vinavyotumiwa kusafisha mazingira.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu jinsi wanavyoweza kuchangia katika usafi wa mazingira.<br>• Mgeni aweza kualikwa ili kusimulia kuhusu mazingira huku wanafunzi wakiandika yaliyo muhimu na kuuliza na kujibu maswali. | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi<br>b) kusikiliza mwalimu kwa makini anaposoma hadithi kuhusu usafi wa mazingira<br>c) kusoma hadithi kuhusu mazingira safi<br>d) kufahamu hadithi aliyosoma na aliyosomewa kuhusu usafi wa mazingira<br>e) kuthamini mazingira safi. | • Mwanafunzi aweza kujadili kuhusu picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kuthibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kufahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Wanafunzi waweza kusoma kama darasa, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Mwanafunzi aweza kutoa muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa.<br>• Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi katika kundi la wawili wawili au darasa zima.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa kupitia kinasasauti.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha, kisha aige usomi | 1) Je, unaweza kukumbuka hadithi gani uliyosoma?<br>2) Je, hadithi unayoweza kukumbuka inahusu nini?<br>3) Je, umeweza kusoma hadithi ngapi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ule.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu mazingira.<br>• Mwanafunzi aweza kuuliza na kujibu maswali kudhihirisha ufahamu. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi kama vile mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa kifupi kinachohusiana na usafi wa mazingira? |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya **haraka** na **polepole**<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **haraka** na **polepole** ili kuimarisha mawasiliano mwafaka<br>b) kutumia **haraka** na **polepole** katika kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano mwafaka<br>c) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya **haraka** na **polepole** ili kujenga usomaji bora | • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia **haraka** na **polepole.**<br>• Mwanafunzi aweza kubainisha matumizi ya vielezi vya jinsi vinavyofunzwa kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia.<br>• Mwanafunzi atazame vitu mbalimbali na avirejelee kwa kutumia **haraka** na **polepole** k.m Mtoto anatembea polepole.<br>• Wanafunzi washiriki katika maigizo wakitumia **haraka** na **polepole** wakiwa darasani.<br>• Mwanafunzi aandike maneno na sentensi kwa kutumia **haraka** na **polepole**. | 1) Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu alivyofanya jambo?<br>2) Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu anavyotembea? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kuandika majina na sentensi kuhusu ndege ili kuimarisha uandishi bora<br>e) Kuchangamkia matumizi ya **haraka** na **polepole** katika mawasiliano. | | |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>mawisiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi<br>ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza<br>hamu ya kujifunza zaidi - kutambua umuhimu wa mazingira. | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya maendeleo endelevu– kupitia kwa kutambua umuhimu wa kudumisha usafi katika mazingira yake. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji katika kuweka mazingira yakiwa safi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental Activities na Hygiene and Nutrition Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kushiriki katika kusafisha mazingira k.m kuokota taka. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>Kuimba nyimbo na kukariri mashairi katika tamasha mbalimbali shuleni kuhamasisha kuhusu usafi wa mazingira. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa usafi wa mazingira katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia **haraka** na **polepole** katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha na ubunifu<br>• anasoma hadithi kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha na ukakamavu | Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira kwa ufasaha<br>• anasoma hadithi kuhusu usafi | Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira<br>• anasoma baadhi ya hadithi vilivyo | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kusikiliza na kuzungumza kuhusu usafi wa mazingira<br>• ana changamoto katika kusoma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anafahamu kwa wepesi aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **haraka** na **polepole** kwa usahihi kila wakati<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ufaavyo. | wa mazingira kwa ufasaha<br><br>• anafahamu aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **haraka** na **polepole** kwa usahihi<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na kwa hati bora. | • anafahamu baadhi ya hadithi alizosoma na kusomewa<br>• anatumia **haraka** na **polepole** kwa wastani<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | hadithi<br><br>• ana changamoto katika kufahamu aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **haraka** na **polepole** katika sentensi<br>• ana changamoto kuandika kisa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Dukani** | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze<br>a) kutambua msamiati wa dukani ili kuutumia katika mawasiliano<br>b) kusoma maneno yanayohusiana na shughuli za dukani ili kujenga usomaji bora<br>c) kueleza maana ya msamiati wa dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d) kutumia msamiati wa dukani katika sentensi sahihi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>e) kuandika maneno yanayohusiana na uuzaji na ununuzi ili kuimarisha stadi ya kusoma | • Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia kadi za maneno kama vile nunua, uza, bei, kilo, mnunuzi, mwuzaji, hasara, faida, pesa, baki, sarafu na noti.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu maana ya maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia picha au michoro.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa dukani.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu uuzaji na ununuzi.<br>• Wanafunzi washiriki katika majadiliano kuhusu umuhimu wa kufanya biashara wakiwa kwenye vikundi. | 1) Mtu anayenunua kitu dukani huitwaje?<br>2) Mtu anayeuza dukani huitwaje?<br>3) Pesa unazorudishiwa unaponunua kitu dukani huitwaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kuthamini shughuli za biashara. | | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotumiwa katika muktadha wa dukani ili kuimarisha ufahamu<br>b) kueleza shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kusikiliza masimulizi kuhusu uuzaji na ununuzi ili kujenga usikivu<br>d) kuthamini biashara katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi asimulie kuhusu shughuli za dukani .<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa anapotoa wasilisho lake kuhusu shughuli za dukani.<br>• Mwanafunzi atambue maneno yanayotumiwa katika muktadha wa dukani kama vile, uuzaji, bei, kilo, ununuzi, hasara, faida, pesa na baki.<br>• Mwanafunzi asikilize kwa makini hadithi zinazosimuliwa kuhusu muktadha wa dukani kwa kutumia maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayohusiana na ununuzi na uuzaji dukani.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu shughuli za dukani katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kuhusu shughuli za dukani.<br>• Mwanafunzi aweza kuigiza kuuza na kununua katika duka la darasani. | 1) Je, umewahi kununua nini dukani?<br>2) Je, ulitumia kiasi gani cha pesa kununua ulichotumwa? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi ili kuwezesha ufahamu<br>b) kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kusikiliza<br>c) kusoma hadithi kuhusu dukani kwa ufasaha ili kujenga usomaji bora<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na | • Mwanafunzi asikilize mwalimu akisoma hadithi ya mwalimu na baadaye kuuliza na kujibu maswali.<br>• Mwanafunzi asome pamoja na wengine darasani, kisha wasome wawili wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Mwanafunzi ajadili picha kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kuhusu kitakachotokea katika hadithi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wengine kujadili msamiati uliotumika katika hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa | 1) Umewahi kusoma hadithi gani kuhusu dukani?<br>2) Je, ni hadithi gani iliyokufurahisha zaidi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | aliyosomewa kuhusu shughuli za dukani ili kupata ujumbe<br>g) kuthamini biashara maishani kama njia moja ya kujitegemea maishani. | kupitia kinasasauti na kisha kuijadili.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu mzima au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi ule.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali.<br>• Mwanafunzi ashiriki kujadili baadhi ya maswali darasani, katika vikundi au wakiwa wawili wawili. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, ni mambo gani utakayoshughulikia katika ukiandika kuhusu dukani? |
| | Sarufi: Matumizi ya alama ya kuuliza(?)<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika | • Mwanafunzi aandike alama ya kuuliza (?).<br>• Mwanafunzi afafanue matumizi ya alama ya kuuliza (?).<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia alama ya kuuliza (?).<br>• Mwanafunzi asome sentensi zilizo na alama ya kuuliza (?). | 1) Je, alama (?) huitwaje?<br>2) Je, utatumia alama (?) unapofanya nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha stadi ya kusoma<br><br>c) kuandika sentensi akitumia alama ya kuuliza (?) katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>d) kuthamini matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika mawasiliano. | • Wanafunzi waweza kushirikishwa kusoma sentensi zinazotumia alama ya kuuliza (?) wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi akitumia alama ya kuuliza (?). | |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>mawisiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi<br>ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza<br>ubunifu – unadhihirishwa na usimulizi na utungaji wa sentensi. | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya maswala ya kifedha katika ujuzi wa kutumia pesa vizuri.<br>stadi za maisha – Kuwa na ujasiri wa kwenda na kufanya maamuzi mwafaka ya ununuzi. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji – Kuweza kuwa mwadilifu katika matumizi ya pesa dukani.<br>ushirikiano – Kufanya kazi katika vikundi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Mathematics Activities, English Activitites. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kuweza kutumwa dukani na wazazi na kutumia pesa inavyofaa. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kushiriki katika maigizo ya shughuli za dukani shuleni<br>kushiriki katika majadiliano kuhusu bidhaa zinazopatikana dukani. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa dukani katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia alama ya kuuliza katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi, | Mwanafunzi, | Mwanafunzi, | Mwanafunzi, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anatambua na kutumia msamiati wa dukani ipasavyo<br>• anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani kwa ubunifu na ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha na ukakamavu<br>• anafahamu kwa wepesi anayosoma au kusomewa<br>• anatumia alama ya kuuliza katika maandishi kila inapohitajika<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, kwa hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. | • anatambua msamiati wa dukani<br>• anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani kwa ufasaha<br>• anafahamu anayosoma au kusomewa<br>• anatumia alama ya kuuliza katika maandishi<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na kwa hati bora. | • anatambua baadhi ya msamiati wa dukani.<br>• anasimulia kisa kuhusu shughuli za dukani<br>• anasoma baadhi maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani<br>• anafahamu baadhi ya mambo anayosoma au kusomewa<br>• anatumia alama ya kuuliza katika baadhi ya sentensi<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | • ana changamoto katika kutambua baadhi ya msamiati wa dukani<br>• ana changamoto katika kusimulia kisa kuhusu shughuli za dukani<br>• ana changamoto katika kusoma baadhi ya maneno, sentensi na hadithi kuhusu shughuli za dukani<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto katika kuakifisha sentensi kwa kutumia alama ya kuuliza<br>• ana changamoto katika kuandika kisa kuhusu mada aliyofunzwa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Ndege Nimpendaye** | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja majina ya ndege mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kutambua msamiati unaotumiwa katika kutunza ndege ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kutumia majina ya ndege katika sentensi sahihi ili kuwezesha mazungumzo<br>d) kutumia msamiati wa kutunza | • Mwanafunzi atazame picha na kuwatambua ndege tofauti tofauti.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati kuhusu ndege.<br>• Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaotumiwa katika kutunza ndege.<br>• Mwanafunzi achore baadhi ya ndege.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya utunzaji wa ndege.<br>• Mwanafunzi atazame michoro na picha za ndege wa nyumbani wakitunzwa. | 1) Ni ndege wepi wanaofugwa?<br>2) Unamtunzaje ndege umpendaye? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ndege katika sentensi ili kuwezesha mazungumzo<br>e) kusoma maneno na sentensi kuhusu ndege ampendaye ili kujenga usomaji bora<br>f) kuandika maneno na sentensi kuhusu ndege ampendaye ili kujenga uandishi bora<br>g) kuthamini utunzaji wa ndege ampendaye. | • Mwanafunzi asome maneno na sentensi katika kadi na chati kuhusu ndege.<br>• Mwanafunzi aandike majina na sentensi kuhusu ndege. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja aina za ndege wa nyumbani anaowajua ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>b) kumtambua ndege ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>c) kusimulia kuhusu ndege ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>d) kusimulia kuhusu jinsi ndege ampendaye anavyotunzwa ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>e) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu utunzaji wa ndege wa nyumbani ili kujenga usikivu<br>f) kuthamini ndege wa nyumbani. | • Mwanafunzi ataje aina za ndege anaowajua.<br>• Mwanafunzi atambue ndege ampendaye.<br>• Mwanafunzi asimulie kuhusu ndege ampendaye katika darasa zima, wakiwa wawili wawili na katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atazame picha za ndege mbalimbali wa nyumbani ili awatambue.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video na picha zinazoashiria utunzaji wa ndege mbalimbali.<br>• Mwanafunzi asimulie jinsi ya kutunza ndege kupitia kwa mgeni mwalikwa.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu jinsi ndege ampendaye anavyotunzwa.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu ndege wawapendao. | 1) Ni ndege gani umpendaye?<br>2) Kwa nini unampenda ndege huyo?<br>3) Unamtunzaje ndege umpendaye? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi aliyosoma au kusomewa ili kuimarisha ufahamu<br>b) kusoma hadithi zinazohusu ndege wa nyumbani ili kujenga usomaji bora<br>c) kusikiliza hadithi zinazohusu ndege wa nyumbani zikisomwa ili kujenga usikivu<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu ndege wanaofugwa ili kupata ujumbe<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi ili kuendeleza ari ya kusoma zaidi. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Wanafunzi washiriki katika kusoma darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kusoma hadithi kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia k.v. tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia msamiati uliotumiwa katika hadithi.<br>• Mwanafunzi anakili majina na sentensi zinazojumuisha majina ndege wa nyumbani.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. | 1) Ni nini unachokiona katika picha?<br>2) Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi?<br>3) Unakumbuka nini kutokana na hadithi uliyosoma?<br>4) Ni kwa nini unampenda ndege wako? |
| | Kuandika ( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi kama vile mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. | 1) Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa gani kinachohusiana na ndege |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | umpendaye? |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya **juu ya** na **chini ya**<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **juu ya** na **chini ya** ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutumia **juu ya** na **chini ya** katika sentensi kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **juu ya** na **chini ya** ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kuandika sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **juu ya** na **chini ya** ili kuimarisha uandishi bora<br>e) kuchangamkia matumizi ya **juu ya** na **chini ya** katika mawasiliano. | • Mwanafunzi asome sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **juu ya** na **chini ya.**<br>• Wanafunzi watunge sentensi zinazorejelea vitu halisi darasani k.m. kitabu kipo juu ya meza wakiwa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kuigiza vitendo vinavyoonyesha **juu ya** na **chini ya.**<br>• Mwanafunzi aweza kukamilisha sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **juu ya** na **chini ya** kwa kurejelea michoro tofauti tofauti akiwa peke yake au katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia tarakilishi kufanyia mazoezi ya matumizi ya **juu ya** na **chini ya.** | 1) Je, ni maneno yapi unayoweza kutumia kurejelea kitu kutegemea mahali kilipo? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawisiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi na wakiwa wawili wawili
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza hadithi msamiati na sauti
kufikiri kwa kina – Kung'amua sifa za ndege ampendaye

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>elimu ya maendeleo endelevu (masilahi ya wanyama – kujali na kutunza ndege) | **Uhusiano na Maadili:**<br>upendo kwa ndege wanaofugwa<br>uwajibikaji katika kutunza ndege. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental Activities, English Activitites. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kutunza ndege na wanyama. |

| Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji: | Mapendekezo ya Tathmini: |
|---|---|
| kushiriki katika vikundi shuleni kama vile chama cha ukulima. | • kuchunguza anavyotumia msamiati wa ndege wanaofugwa katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia **juu ya** na **chini ya** katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kusimulia hadithi kwa ukakamavu na ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu ndege ampendaye kwa wepesi na ufasaha<br>• anafahamu kwa wepesi hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **juu ya** na **chini ya** kutunga sentensi sahihi zenye ubunifu wa hali ya juu<br>• anaandika kisa kwa ubunifu, mtiririko, hati nadhifu na kwa haraka. | Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kusimulia hadithi kwa ufasaha<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu ndege ampendaye kwa ufasaha<br>• anafahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **juu ya** na **chini ya** kutunga sentensi sahihi<br>• anaandika kisa kwa mtiririko na hati bora. | Mwanafunzi,<br>• anasikiliza na kusimulia hadithi<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu ndege ampendaye<br>• anafahamu baadhi ya hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **juu ya** na **chini ya** kutunga sentensi sahihi<br>• anaandika kisa kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kusimulia hadithi<br>• ana changamoto katika kusoma baadhi ya maneno, sentensi na hadithi kuhusu ndege ampendaye<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **juu ya** na **chini ya** kutunga sentensi sahihi<br>• ana changamoto katika kuandika kisa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Sokoni** | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati unaohusiana na shughuli za sokoni ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma msamiati wa sokoni ili kujenga usomaji bora<br>c) kufahamu maana ya msamiati unaotumiwa sokoni ili kuwezesha mawasiliano<br>d) kutunga sentensi akitumia msamiati wa sokoni ili kuimarisha mawasiliano<br>e) kuandika maneno na sentensi akitumia msamiati wa sokoni ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>f) kuthamini shughuli za sokoni. | • Mwanafunzi asome maneno kuhusu soko kwenye kadi na chati.<br>• Mwanafunzi afafanue maana ya msamiati wa sokoni k.v mkokoteni, vibanda, ratili, bidhaa, risiti, dalali, mnunuzi, muuzaji na mchuuzi).<br>• Mwanafunzi achore vitu vipatikanavyo sokoni.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama picha au video za vitu vya sokoni zikiambatanishwa na sauti na maneno.<br>• Mwanafunzi aambatanishe majina na vitu vipatikanavyo sokoni.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza nafasi katika sentensi kwa maneno yanayotumiwa sokoni.<br>• Mwanafunzi anakili msamiati kuhusu shughuli za sokoni.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia msamiati kuhusu shughuli za sokoni. | 1) Ni maneno yapi au msamiati upi unaotumika sokoni?<br>2) Je, unaweza kuchora bidhaa gani zinazopatikana sokoni? |
| | Kusikiliza na kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja vitu vinavyopatikana sokoni katika kuendeleza mazungumzo<br>b) kutaja watu wanaopatikana sokoni katika kuendeleza mazungumzo<br>c) kusikiliza maelezo kuhusu sokoni ili kujenga usikivu | • Mwanafunzi ataje vitu vipatikanavyo sokoni k.v mkokoteni, vibanda, ratili, bidhaa na risiti.<br>• Mwanafunzi ataje watu wanaopatikana sokoni kama vile dalali, mnunuzi, muuzaji na mchuuzi.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kuigiza michezo kuhusu shughuli zinazoendeshwa sokoni.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kujadili kuhusu shughuli za sokoni.<br>• Mwanafunzi ajadili michoro, chati na picha kuhusu sokoni. | 1) Ni watu wepi wanaopatikana sokoni?<br>2) Ni vitu gani vinavyopatikana sokoni?<br>3) Soko lina umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kueleza shughuli zinazoendeshwa sokoni ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>e) kueleza umuhimu wa soko ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>f) kuthamini shughuli za sokoni kama njia moja ya kujipatia riziki. | • Mwanafunzi atoe maelezo kuhusu umuhimu wa soko.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu shughuli za sokoni.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video na picha kuhusu shughuli za sokoni.<br>• Mwanafunzi asimulie kisa chochote alichoshuhudia kuhusu sokoni pekee, akiwa katika kikundi au wakiwa wawili. | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi ili kuwezesha ufahamu<br>b) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu sokoni ili kujenga usikivu<br>c) kusoma hadithi kuhusu sokoni ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma au kusomewa kuhusu sokoni ili kupata ujumbe<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi ili kujenga ari ya kuendeleza ujifunzaji. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ashiriki kusoma darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akisoma hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia vifaa vya kiteknolojia huku mwanafunzi akikumbushwa kusikiliza kwa makini.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kupanga upya sentensi zilizoparaganywa zinazohusu sokoni katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyoisoma.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na | 1) Ni watu wepi wametajwa katika hadithi?<br>2) Ni vitu gani vimetajwa katika hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hadithi. | |
| | Kuandika<br>( *Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi<br>b) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | • Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br>• Mwanafunzi aeleze mambo yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br>• Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwalimu.<br>• Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | 1) Je, ni mambo yapi unayofaa kuzingatia unapoandika kisa?<br>2) Je, unaweza kuandika kisa kipi kinachohusiana na mada ya sokoni? |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya **ndani ya** na **nje ya**<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **ndani ya** na **nje ya** ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutumia **ndani ya** na **nje ya** katika sentensi kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **ndani ya** na **nje ya** ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kuandika sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **ndani ya** na **nje ya** ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>e) kuchangamkia matumizi ya **ndani ya** na **nje ya** katika maawasiliano. | • Mwanafunzi asome sentensi zinazodhihirisha matumizi **ndani ya** na **nje ya.**<br>• Mwanafunzi atunge sentensi zinazorejelea vitu halisi darasani k.m. kitabu kimo **ndani ya** kabati; Mwanafunzi yupo **nje ya** darasa; katika vikundi.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kuigiza vitendo vinavyoonyesha **ndani ya** na **nje ya**.<br>• Mwanafunzi aweza kukamilisha sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **ndani ya** na **nje ya** kwa kurejelea michoro tofauti tofauti akiwa peke yake au katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kufanya mazoezi ya kutumia **ndani ya** na **nje ya** kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia. | 1) Je, ni nini kinyume cha **ndani ya**? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi<br>ujuzi wa kidijitali - matumizi ya teknolojia katika kujifunza<br>hamu ya kutaka kujua zaidi - kusoma hadithi. | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya masuala ya kifedha – kujadili umuhimu wa sokoni. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uadilifu katika shughuli za sokoni<br>umoja – Hamna biashara inayoweza kunawiri pasipo na umoja<br>heshima ni muhimu popote watu wanapoingiliana hasa sokoni<br>uwajibikaji – Mwenye biashara na mnunuzi sharti wawajibike katika shughuli husika. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Mathematics Activities, English Activitites, Environmental Activities, Literacy and Indigeneous languages | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kusaidia jamii katika shughuli zinazohusu soko. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kushiriki katika katika kuigiza shughuli za sokoni. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotumia msamiati wa sokoni katika mawasiliano<br>• kuchunguza anavyotumia **ndani ya** na **nje ya** katika mawasiliano<br>• kuchanganua anavyojibu maswali ya kusema na ya kuandika<br>• kuchunguza ufahamu wake wa hadithi aliyosoma au kusomewa<br>• kuhakiki anavyosoma na kusimulia hadithi<br>• kufuatilia mwandiko wake. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatambua na kutumia msamiati unaopatika sokoni<br>• anasimulia visa kuhusu sokoni kwa ubunifu na ukakamavu<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu sokoni kwa ufasaha<br>• anatumia **ndani ya** na **nje ya** kutunga sentensi sahihi zenye ubunifu wa hali ya juu<br>• anaandika kisa kinachohusiana na sokoni kwa ubunifu, mtiririko, hati nadhifu na kwa kasi ifaayo. | Mwanafunzi,<br>• anatambua msamiati unaopatika sokoni<br>• anasimulia visa kuhusu sokoni kwa ukakamavu<br>• anasoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu sokoni<br>• anatumia **ndani ya** na **nje ya** kutunga sentensi sahihi<br>• anaandika kisa kinachohusiana na sokoni kwa mtiririko na hati bora. | Mwanafunzi,<br>• anatambua baadhi msamiati unaopatika sokoni<br>• anasimulia baadhi ya visa kuhusu sokoni<br>• anasoma baadhi ya maneno, sentensi na hadithi kuhusu sokoni<br>• ana changamoto kiasi katika kutumia **ndani ya** na **nje ya** kutunga sentensi sahihi<br>• anaandika kisa kinachohusiana na sokoni kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutambua msamiati unaopatika sokoni<br>• ana changamoto katika kusimulia visa kuhusu sokoni<br>• ana changamoto katika kusoma maneno, sentensi na hadithi kuhusu sokoni<br>• ana changamoto katika kutumia **ndani ya** na **nje ya** kutunga sentensi sahihi<br>• ana changamoto katika kuandika kisa kinachohusiana na sokoni. |